**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Anwani ya Simu: "ELIMU" Simu:
026 296 35 33
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S.L.P 10,
**40479 DODOMA**

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb.Na.CA.229/238/01/57**

**28 Februari, 2023.**

Mwenyekiti,

TAMONGSCO,

S.L.P 63088,

**DODOMA.**

Katibu Mtendaji,

Christian Social Services Commission (CSSC),

S.L.P 1454,

**DAR ES SALAAM.**

Katibu Mtendaji,

Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA),

S.L.P 21422,

**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,

Tanzania Association of Private Investors in Education (TAPIE),

S.L.P 13346,

**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,

Baraza la Sunnar Tanzania (BASUTA),

S.L.P 8581,

**DAR ES SALAAM.**

Mkurugenzi,

Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET),

S.L.P 13547,

**DAR ES SALAAM.**

**WARAKA WA ELIMU NA. 03 WA MWAKA 2023**
**KUHUSU UTAYARISHAJI NA UPATIKANAJI WA VIFAA VYA KUJIFUNZIA NA KUFUNDISHIA**

Tafadhali rejea mada husika hapo juu.

2. Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hauwezi kuwa fanisi bila upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya kutosha na vyenye ubora stahiki. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia ni nyenzo muhimu katika kuandaa wahitimu wa elimu katika ngazi mbalimbali wenye umahiri stahiki na maadili yanayoakisi mila, desturi na tamaduni za nchi yetu. Katika zama za utandawazi, suala la upatikanaji wa vifaa bora vya kufundishia na kujifunzia katika shule na vyuo vya ualimu linapaswa kufanyiwa kazi kwa umakini mkubwa kutokana na ukweli kwamba, katika zama hizi, vitabu na vifaa mbalimbali vilivyo katika nakala ngumu na vya kielektroniki kutoka ndani na nje ya nchi vinaandaliwa na kusambazwa kwa njia mbalimbali kupitia taasisi na watu binafsi. Kwa sababu hiyo, kuna haja ya kuweka mfumo thabiti wa uhakiki wa maudhui ya vitabu na vifaa hivyo ili kuhakikisha kwamba vitabu na vifaa vinavyoingizwa na kutumika shuleni na vyuo vya ualimu vinawajengea wahitimu wetu umahiri na maadili stahiki.

3. Kwa kuzingatia umuhimu huo, mwaka 2014 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Wakati huo ikiitwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi) iliandaa na kutoa **Waraka wa Elimu Na.4 wa Mwaka 2014 kuhusu Utayarishaji wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia**. Waraka huo ulianza kutumika tarehe 1/9/2014 ambapo Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ilipewa jukumu la uandishi na uchapishaji wa vitabu vya kiada kwa ngazi za Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Aidha, TET ilipewa jukumu la uratibu wa upatikanaji wa vitabu vya ziada na vifaa vingine vya kielimu vilivyopaswa kuandaliwa na wachapaji binafsi. Vitabu vyote vya kiada na ziada kwa matumizi katika Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu vilitakiwa kupata ithibati kutoka kwa Kamishna wa Elimu.

4. Pamoja na kutolewa kwa Waraka wa Elimu Na.4 wa Mwaka 2014, bado changamoto za ubora na matumizi sahihi ya vitabu na vifaa vingine vya elimu zimeendelea kujitokeza. Changamoto hizo zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku kutokana na utandawazi ambao umeongeza uwezekano wa uingizaji huria wa vitabu na vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia katika nchi kwa ujumla na hususan katika shule na vyuo vya ualimu.

5. Kwa kuzingatia maelezo hayo, Wizara imeandaa Waraka huu ili kuhakikisha kwamba vitabu na vifaa mbalimbali vya kielektroniki na nakala ngumu vinavyoingizwa nchini kwa upande mmoja na shuleni na vyuo vya ualimu kwa upande mwingine, vina maudhui yanayoendana na maadili, mila, desturi na tamaduni zetu. Kwa Waraka huu, suala la uandaaji, uchapaji na usambazaji wa vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia litatekelezwa kama ifuatavyo:

i. Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA), kwa kutumia mamlaka yake kisheria, iandae mfumo wa kudhibiti vitabu na vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia vinavyoingizwa nchini ili kuhakikikisha kwamba maudhui ya vitabu na vifaa hivyo yanaendana na maadili, mila, desturi na tamaduni zetu. Aidha, BOHUMATA iweke mfumo wa ukaguzi wa vitabu na vifaa mbalimbali vilivyo katika maduka ya vitabu na maktaba za shule na vyuo vya ualimu. Ukaguzi huo ufanyike pia katika Maktaba zote za Umma na zisizokuwa za Umma;

ii. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) iendelee kutekeleza majukumu yake kama ilivyoelekezwa katika **Waraka wa Elimu Na. 4 wa Mwaka 2014 kuhusu Utayarishaji wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia;**

iii. Wathibiti Ubora wa Shule wafanye ukaguzi wa mara kwa mara wa vitabu na vifaa mbalimbali vya kujifunzia na kufundishia vilivyo katika shule na maktaba zake na vyuo vya ualimu kwa lengo la kudhibiti maudhui yasiyofaa;

iv. Kamati za Shule ya Msingi na Bodi za Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu zifanye ufuatiliaji wa vitabu na vifaa mbalimbali vya kujifunzia na kufundishia vilivyo katika shule na vyuo husika ili kuhakikisha kwamba maudhui ya vifaa na vitabu hivyo yanaendana na maadili, mila, desturi na tamaduni zetu;

v. Walimu na Wakufunzi wa Taaluma katika shule na vyuo vya ualimu mtawalia waweke utaratibu wa kukagua vitabu na vifaa mbalimbali vya kujifunzia na kufundishia walivyonavyo wanafunzi ili kudhibiti uingizwaji na matumizi ya vitabu na vifaa vinavyokwenda kinyume na maadili, mila, desturi na tamaduni zetu;

vi. Endapo shule au chuo cha ualimu kitapokea msaada wa vitabu au vifaa vyovyote vya kujifunzia, itatakiwa kushirikisha Wathibiti Ubora wa Shule katika eneo husika ili kufanya ukaguzi wa vitabu au vifaa hivyo kabla ya kuanza kutumika katika shule au chuo husika; na

vii. Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA) iweke utaratibu wa kukagua vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia inavyopokea kama msaada ili kuhakikisha kwamba vitabu na vifaa hivyo vina maudhui stahiki.

6. Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Machi, 2023.

7. Nawatakia utekelezaji mwema.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**KAMISHNA WA ELIMU**

**Nakala:** Mkurugenzi Mkuu - Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania

Mkurugenzi Mkuu - Taasisi ya Elimu Tanzania

Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule Kanda na Wilaya

**TANZANIA BARA**